**TAARIFA YA KAIMU AFISA MTENDAJI MKUU WA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI (MSCL) PHILEMON BAGAMBILANA WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA MIRADI YA UKARABATI WA NEW VICTORIA HAPA KAZI TU, NEW BUTIAMA HAPA KAZI TU, CHELEZO PAMOJA NA UTIAJI SAINI MIKATABA MITANO YA UJENZI WA MELI MPYA NNE NA UKARABATI WA MELI MOJA YA MV. UMOJA KATIKA BANDARI YA MWANZA KUSINI, ZIWA VICTORIA TAREHE 15 JUNI, 2021**

**Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha taarifa kuhusu miradi mitatu uliyoizindua muda mfupi uliopita pamoja na miradi mitano ambayo muda mfupi ujao utashuhudia utiaji saini wa mikataba yake;

Awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali na Neema ya kusimama mbele ya hadhara hii:

**Mheshimiwa Rais**

Miradi ya Ukarabati wa meli za "New Victoria Hapa Kazi Tu" na "New Butiama Hapa Kazi Tu ilianza kutekelezwa mwezi Januari, 2019 na mkandarasi aitwaye KTMI Co. Ltd kutoka nchini Korea Kusini kwa kushirikiana na kampuni ya Yuko's Enterprise (EA) ya Tanzania.

Miradi yote miwili imekamilika kwa wakati kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 27.6 ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 22.7** ni kwa ajili ya ukarabati wa New Victoria Hapa Kazi Tu na **Shilingi Bilioni 4.9** ni kwa ajili ya Ukarabati wa meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu. Meli ya "New Victoria Hapa Kazi Tu" ina uwezo wa kubeba abiria 1,200 na mzigo tani 200 wakati "New Butiama Hapa Kazi Tu" ina uwezo wa kubeba abiria 200 na mzigo tani 100.

Aidha, mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Chelezo nao ulianza kutekelezwa mwezi Januari, 2019 na kampuni ya STX Engine Co. Ltd kwa kushirikiana na kampuni ya Saekyung Co. Ltd. zote kutoka nchini Korea Kusini. Mradi huu ambao mkataba wake ulikuwa ni wa mwaka mmoja tayari umeshakamilika na Chelezo hicho tayari kimeanza kutumika kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu.

Chelezo hiki kina uwezo wa kuhudumia meli yenye uzito wa tani 4,000 na ndicho Chelezo chenye uwezo mkubwa kuliko vyote katika Ziwa Victoria. Gharama ya ujenzi wa Chelezo hiki kwa mujibu wa mkataba ni **Dola za Marekani 15,814,747 sawa na Shilingi bilioni 36.4**.

**Mheshimiwa Rais**,

Ukarabati uliofanyika katika meli hizi, umehusisha sehemu zote muhimu za meli hizo na hivyo kuhuisha hali zake kiasi cha kuweza kutumika kwa miaka mingine 30 ijayo. Ukarabati huo umejumuisha ufungaji wa injini mpya katika meli zote mbili, majenereta mapya kwa ajili ya kuzalisha umeme, vifaa vya kuongozea meli hizo (navigation equipment) na kinyakuzi kipya (crane) (kwa upande wa meli ya ***New Victoria Hapa Kazi Tu***). Pia, ukarabati huo umehusisha maboresho katika sehemu za kukaa abiria (accommodation facilities) ambapo vimefungwa viti vipya na vya kisasa na kuondoa mabenchi pamoja na kufanya maboresho katika sehemu za kulala abiria na wafanyakazi wa melini (mabaharia) ili kuwawezesha kusafiri kwa uhakika na salama.

Maboresho mengine yaliyofanyika yamehusisha ufungaji wa mfumo mpya wa umeme (new wiring system) na uwekaji wa vifaa vipya vya usalama na uokozi (Safety and Rescue gears).

Kwa ujumla maboresho yaliyofanyika ni makubwa sana kiasi cha kuzifanya meli hizo kuonekana kuwa mpya na za kisasa zaidi huku zikiwa na kasi kubwa tofauti na hapo awali kufuatia kufungwa kwa injini kubwa na za kisasa na ndio sababu ya kubadilisha majina yake na kuitwa New Victoria Hapa Kazi Tu na New Butiama Hapa Kazi Tu.

Meli zote mbili zilianza kutoa huduma tena tangu tarehe 16 Agosti, 2020 ambapo meli ya New Victoria inafanya safari zake kati ya Mwanza na Bukoba kupitia bandari ya Kemondo na New Butiama inafanya safari zake kila siku kati ya Mwanza na Nansio – Ukerewe.

**Mheshimiwa Rais,**

Miradi yote hii imegharimiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100** kwa kutumia fedha ya walipa Kodi. Tuna kila sababu ya kukushukuru wewe **Mheshimiwa Rais** pamoja na Serikali yako unayoiongoza kwa kuendelea kuwekeza katika sekta ya Usafiri kwa njia ya maji ili kuwaletea maendeleo wananchi wanaotegemea usafiri huu kwa ajili ya kuendesha shughuli zao na hivyo kukuza Uchumi wao na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Rais,**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli inayoongozwa na **Mhandisi Profesa Zacharia Mganilwa**, nakushukuru kwa kukubali pia leo hii kuja kushuhudia utiaji saini wa jumla ya mikataba mitano (5) kama ifuatavyo:

i. **Mkataba wa Ujenzi wa meli mpya katika Bahari ya Hindi;**

Huu ni mradi wa Ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo katika Bahari Hindi. Mzabuni wa kutekeleza mradi huu ni Kampuni ya YUTEK GEMI INSA. SAN LTD ya Uturuki kwa gharama za Dola za Marekani 55,200,000.00.

ii. **Mradi wa Ujenzi wa meli ya mizigo katika Ziwa Victoria;**

Mradi wa Ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria. Mzabuni wa kutekeleza mradi huu ni Kampuni ya YUTEK GEMI INSA.SAN LTD ya Uturuki kwa gharama za Dola za Marekani 35,950,000.00.

iii. **Mradi Ujenzi wa Meli ya mizigo na abiria katika Ziwa Tanganyika;**

Mradi wa Ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika. Mzabuni wa kutekeleza mradi huu ni Kampuni ya YUTEK GEMI INSA.SAN LTD ya Uturuki kwa gharama za Dola za Marekani 44,500,000.00.

iv. **Mradi wa Ujenzi wa meli ya mizigo katika Ziwa Tanganyika;**

Mradi wa Ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo kiasi cha tani 4,000 katika Ziwa Tanganyika. Mzabuni wa kutekeleza mradi huu ni

Kampuni ya YUTEK GEMI INSA.SAN LTD ya Uturuki kwa gharama za Dola za Marekani 42,500,000.00

v. **Mradi wa Ukarabati wa meli ya MV. Umoja katika Ziwa Victoria**

Mradi wa Ukarabati mkubwa wa meli MV.Umoja inayobeba mabehewa katika Ziwa Victoria. Mzabuni wa kutekeleza mradi huu ni Kampuni ya SM SOLUTION CO.LTD. ya Korea Kusini kwa gharama za Dola za Marekani 8,422,840.00.

Miradi yote hii mitano inagharimu kiasi cha Dola za Kimarekani **186,572,840.00** sawa na Shilingi za Kitanzania **438,839,842,692.40** ambazo ni fedha za walipa kodi.

**Mheshimiwa Rais,**

Pamoja na miradi tajwa hapo juu, pia Kampuni yetu inaendelea na utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria unaogharimu **Shilingi bilioni 89** ambao unatekelzwa na Kampuni ya GAS Entec ikishirikiana na Kangnam kutoka Korea Kusini pamoja na SUMA JKT.

Ujenzi wa meli hii ulianza rasmi mwezi Januari, 2019 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Aprili, 2022 kwa mujibu wa Mkataba huku meli hiyo ikiwa na uwezo wa kubeba jumla ya abiria 1,200, tani 400 za mizigo magari madogo 20 na magari makubwa 3.

**Mheshimiwa Rais**,

Haya kwetu wana MSCL ni mafanikio makubwa sana na hivyo Mheshimiwa Rais, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wote pamoja na Wataalam kwa ujumla, tunapenda kutoa

shukrani zetu kwako mwenyewe, Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Waziri, **Mhandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho (Mb), Katibu Mkuu-Uchukuzi Bw. Gabriel Joseph Migire** pamoja na maafisa kadhaa wa Wizara ambao kwa kiasi kikubwa wameshiriki katika kufanikisha utekelezaji wa miradi hii.

Aidha, tunapenda kulishukuru Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) chini ya Usimamizi wa Mkuu wa Majeshi, **Jenerali Venance Mabeyo** kwa kutupatia wataalamu wa kusimamia miradi hii kutoka Kamandi ya Wanamaji. Pia tunaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa mchango wake mkubwa katika kuikwamua Kampuni yetu kutoka katika hali ngumu ya kiutendaji.

Aidha, tunapenda kutoa shukrani za kipekee kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa inayoongozwa na Mkuu wa Mkoa **Mheshimiwa Mhandisi Robert Gabriel Luhumbi** ambao wamekuwa nasi bega kwa bega ili kuhakikisha kuwa miradi hii inatekelezwa kama ilivyopangwa.

**Mheshimiwa Rais,**

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba nikupongeze wewe na Serikali yako inayoiongoza, kwa Kazi kubwa ya ujenzi wa Taifa ikiwemo dhamira ya kuhakikisha kuwa miundombinu ya usafirishaji inakuwa kichocheo cha ukuuaji wa uchumi wa nchi. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kukupa maono na afya njema ili kuifikisha Tanzania katika viwango vya juu kiuchumi.

**Mheshimiwa Rais**, naomba kuwasilisha.